

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA

(Barua zote ziandikwe kwa Msimamizi wa Uchaguzi)

MKOA WA RUVUMA

Simu : 025 2602970

Nukushi : 025 2602474

Barua pepe: [info@songeamc.go.tz](mailto:info@songeamc.go.tz)

Unapojobu tafadhali taja:

Kumb. Na. SO/MC/E.20/13/4



UKUMBI WA MANISPAA,  
S. L. P. 14,  
SONGEA.

Tarehe: 23 Septemba, 2019

**Kwa Wakazi Wote;**  
**Halmashauri ya Manispaa ya Songea**

## **MAELEKEZO KUHUSU UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA UTAKAOFANYIKA TAREHE 24 NOVEMBA, 2019**

Kwa kuzingatia Kanuni ya 9 ya Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa katika Mamlaka za Miji za Mwaka 2019; Msimamizi wa Uchaguzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea anawatangazia wananchi kuwa **tarehe 24 Novemba, 2019** kufanyika Uchaguzi wa serikali za mitaa na kwamba masuala ya msingi ya kuzingatia kwa wananchi wote ni kama yafuatayo:-

- 1) Uchaguzi utafanyika tarehe 24 Novemba, 2019**
- 2) Wakazi wote wenye sifa ya kupiga kura wanatakiwa kujitokeza kwa wingi kushiriki Uchaguzi kwa kuijandikisha kwenye orodha ya wapiga kura kuanzia Tarehe 08 hadi **14 mwezi Oktoba 2019** kila siku kuanzia **saa 2.00 asubuhi** hadi **saa 12.00 jioni**. Kila mkazi anatakiwa kuijandikisha kwenye Mtaa anaoishi.**
- 3) Uchaguzi utafanyika kwenye kituo ulichojiandikisha na upigaji kura utaanza **saa 02.00 asubuhi** mpaka **saa 10.00 jioni**. Baada ya kupiga kura mtu yejote asiyetajwa Kusimamia Uchaguzi **Hataruhusiwa** kubaki katika eneo la kituo cha kupigia kura**

- 4)** Wakazi wote wenye umri wa kuanzia miaka 21 wanaotaka kugombea nafasi za Uenyekiti wa Mtaa na Ujumbe wa Serikali ya Mtaa kujitokeza kuchukua fomu za kugombea kwenye Ofisi ya Msimamizi Msaidizi wa Mtaa (Ofisi ya Mtendaji wa Mtaa wako) kila siku kuanzia saa 1.30 asubuhi hadi saa 10.00 jioni kuanzia tarehe 29 Oktoba, 2019 hadi tarehe 04 Novemba 2019. Kumbuka wagombea wote wanatakiwa kudhaminiwa na vyama vyao vya Siasa.
- 5)** Fomu za wagombea walioteuliwa zitabandikwa siku ya tarehe 05 Novemba, 2019 **kuanzia saa 2.00 asubuhi** hadi **saa 10.00 jioni** katika ofisi ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi .
- 6)** Pingamizi dhidi ya uteuzi wa wagombea zitawasilishwa na kusikilizwa na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kila siku kuanzia Tarehe 05-06 Novemba 2019.
- 7)** Kamati ya Rufaa itapitia, kusikiliza na kutoa uamuza wa Rufaa za wagombea kuanzia tarehe 05 Novemba 2019 hadi tarehe 07 Novemba 2019.
- 8)** Kampeni za uchaguzi zitafanyika kila siku kuanzia tarehe 17 Novemba 2019 hadi 23 Novemba 2019 saa 2.00 asubuhi hadi saa 12.00 jioni
- 9) Sifa za Mpiga kura**

Ni raia wa Tanzania, ana umri wa miaka 18 au zaidi, ni mkazi wa kawaida wa eneo la Mtaa, Mwenye akili timamu na awe amejiandikisha kupiga kura katika Mtaa husika.

**Mtu hataruhusiwa kupiga kura ikiwa-;**

Si raia wa Tanzania, Hajatimiza umri wa miaka kumi na nane, Si mkazi wa kawaida wa eneo la Kitongoji, na mwenye ugonjwa wa

akili uliothibitishwa na Daktari anayetambulika na Serikali au bodi ya utabibu.

## 10) Sifa za Mgombéa

Mkazi ye yote wa Mtaa anaweza kugombea uenyekiti wa Mtaa au ujumbe wa Serikali ya Mtaa ikiwa:-

- Ni raia wa Tanzania, Ana umri wa miaka Ishirini na moja (21) au zaidi, ana uwezo wa kusoma na kuandika Kiswahili au Kiingereza, Ana kipato halali cha kumwezesha kuishi, Ni mkazi wa kawaida wa eneo la Mtaa, Ni mwanachama na amedhaminiwa na Chama cha Siasa, hajawahi kupatikana na Hatia kwa kosa la utovu wa Uhaminifu au kuhukumiwa adhabu ya Kifungo cha miezi sita au zaidi au adhabu ya kifo na hana ugonjwa wa akili uliothibitishwa na Daktari anayetambulika na Serikali au Bodi ya Utabibu.

*Msimamizi wa Uchaguzi anavikumbusha vyama vya siasa na wadau wote wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa kuzingatia Sheria, Kanuni, Miongozo na Maelekezo yote wakati wote wa maandalizi ya uchaguzi.*

*Lewis Yohana Mnyambwa*  
**MSIMAMIZI WA UCHAGUZI**  
**HALMASHAURI YA MANISPAA SONGEA**

**Nakala;**

Mbao zote za Matangazo kwenye Tarafa, Kata na Mitaa.